
#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 21

Januari - Machi 2026

## NDANI...




06 HESLB na CIT zasaini makubaliano ya mashirikiano



09 HESLB yatuzwa taasisi kinara matumizi ya mifumo kidigitali




# HESLB Yazindua "BWANABOOM" Kuboresha huduma kwa wadau

**Dodoma, Jumatano, 28, Januari 2026**

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imezindua rasmi mfumo wezeshi wa huduma kwa wateja kwa kutumia akili unde unaojulikana kwa jina la BWANABOOM, unaolenga kuboresha na kuharakisha utoaji wa huduma kwa wadau wa elimu nchini kwa saa 24 kila siku.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), Profesa Daniel Mushi, alikuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo uliofanyika katika ofisi za Makao Makuu ya HESLB jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB. Wengine walioshuhudia tukio hilo ni pamoja na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Maryam Ismail, Menejimenti ya HESLB, wawakilishi wa wanafunzi kutoka Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha St. John's na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Dodoma.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Prof. Mushi aliisifu HESLB kwa juhudi zake za kuendelea kubuni na kuendeleza mifumo ya kiteknolojia ambayo imekuwa chachu ya kuboresha utoaji wa huduma kwa ufanisi kwa wananchi na wadau wa elimu nchini. "Leo tunaongeza huduma ya Akili Unde 'BWANABOOM' kama njia nyingine muhimu ya kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wadau kuwasiliana moja kwa moja na HESLB kwa njia hii ya kidigitali. Hili ni jambo la kujivunia na linapaswa kuigwa na taasisi nyingine nchini", alisema Prof. Mushi.

Naibu Katibu anayesimamia Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, alipongeza HESLB kwa maono na ubunifu wake katika utoaji wa huduma kwa Watanzania, hususan wanafunzi wa elimu ya juu, akibainisha kuwa mfumo huo wa huduma kwa kutumia akili unde ni hatua muhimu katika safari ya mageuzi ya kidigitali kwenye sekta ya elimu.

Aidha, Prof. Mushi alisisitiza kuwa kutokana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, ni muhimu kwa HESLB kuendelea kuboresha huduma zake, kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa, pamoja na kuandaa mikakati itakayowezesha matumizi ya lugha ya ishara ili kuwahudumia ipasavyo wadau wenye mahitaji maalumu.

"Ni muhimu mkumbuke kuwa teknolojia inabadilika kwa kasi kubwa … ninatoa wito kwenu kuendelea kuboresha huduma zitolewazo kupitia BWANABOOM, kuhakikisha usalama wa taarifa binafsi unazingatiwa kikamilifu, kuendelea kupima kiwango cha kuridhika kwa wateja ili kuboresha zaidi huduma, na kuangalia uwezekano wa kuanzisha lugha ya ishara ya kidigitali, ili Watanzania wenye ulemavu wa kusikia, waweze kupata huduma kupitia 'BWANABOOM', amesisitiza Prof. Mushi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alisema ubunifu wa BWANABOOM ni sehemu ya safari ya kimkakati ya taasisi hiyo anayoiongoza katika kuboresha huduma kwa wateja kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa lengo la kuongeza ufanisi, uwazi na urahisi wa upatikanaji wa taarifa. Naye Bi. Jaqueline Humbaro ambaye ni Rais wa Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu Dodoma (UDOM) na mwanafunzi wa Sheria, mwaka wa nne, alisifu ubunifu huo na kuahidi kuwashirikisha na kuwahimiza wanafunzi wenzake kuutumia ili kunufaika na huduma hiyo mpya na ya kisasa.

Mfumo wa BWANABOOM unatarajiwa kurahisisha utoaji wa huduma kwa wadau wa elimu, kupunguza gharama za usafiri na muda, huku taarifa muhimu zikisogezwa karibu zaidi na wananchi kupitia tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz) na akaunti za mikopo za wanafunzi maarufu 'SIPA'. Mfumo huu unaonesha dhamira ya HESLB katika kutumia teknolojia ya akili unde kama nyenzo ya kiteknolojia ya kuboresha maendeleo ya elimu nchini.

## JAMBO LETU



Jaqueline Msuya
*Mhariri*

# RC Dar:
## Wanawake ni nguzo ya maendeleo ya taifa



**Dar es Salaam, Jumapili, Machi 08, 2026**

Watumishi wanawake wa HESLB wameungana na maelfu ya wanawake kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani katika Viwanja vya Mburahati - Barafu, ambapo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo yaliyosheheni ujumbe wa haki, usawa na uwezeshaji wa wanawake.

Katika hotuba yake, Mhe. Chalamila alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuweka mazingira rafiki yanayowezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam alisisitiza kuwa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yana mchango mkubwa katika kujenga mshikamano, kuhamasisha usawa wa kijinsia na kuongeza fursa za uwezeshaji kwa wanawake katika nyanja mbalimbali.

"Maadhimisho haya yanatukumbusha kuwa wanawake ndio nguzo kubwa ya maendeleo na mambo mengi katika taifa letu. Tunapaswa kuyaona kama jukwaa la kuimarisha umoja, kujenga hamasa na kusukuma mbele ajenda ya usawa wa kijinsia," alisema, Mhe. Chalamila na kuwakumbusha wanawake kuwa wana wajibu mkubwa wa kujiimarisha kiuchumi kwa kufanya kazi kwa bidii na kutumia ipasavyo fursa zinazopatikana.

"Maadhimisho haya yatukumbushe kuwa wanawake tuna wajibu mkubwa sana wa kujiimarisha kiuchumi kwa kufanya kazi kwa juhudi. Kila mwanamke anapaswa kufanya mambo kulingana na uwezo na kipato chake, na si kuishi kwa kuiga maisha ya wengine," alisisitiza Mhe. Chalamila.

Aidha, katika nasaha zake kwa jamii, aliwataka wanaume na wanawake wanaopata mafanikio katika maisha yao kuhakikisha wanawakumbuka wazazi wao, hususan mama zao, kwa kuwasaidia na kuboresha maisha yao.

Kwa upande mwingine, Mhe. Chalamila alipendekeza maboresho katika maadhimisho ya mwaka ujao kwa kufikiria kujumuisha kliniki maalum kwa ajili ya wanawake, itakayosaidia kutoa huduma mbalimbali za afya, ushauri na elimu kuhusu sheria na ustawi wa wanawake.

Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani ambayo kwa mwaka huu yameongozwa na kauli mbiu isemayo: "Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050", kwa Mkoa wa Dar es Salaam yalifanyika siku ya Jumapili, Machi 8, 2026 katika Viwanja vya Mburahati Barafu.

# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Amani Kakana

**Mhariri**
Jaqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Ramadhan Namaru

**Designer**
Abdul K. Msangi
+255 621 579 833

**Photographer**
Edwin Msuya
+255 688 410 683

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067 577
+255 739 067 577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# ... sauti ya uwajibikaji na uendelevu

**Dar es salaam, Jumanne, Machi 10, 2026**

Nakukaribisha katika toleo la 21 la jarida la mtandao, HESLB Yako, jukwaa linaloangazia simulizi za matumaini, uwajibikaji na maendeleo ya elimu ya juu nchini.

Ni dhahiri kuwa elimu ni nguzo ya maendeleo ya kila taifa na ndiyo maana HESLB imeendelea kuwa daraja linalounganisha ndoto za vijana na uhalisia wa kuzitimiza. Hata hivyo, nyuma ya kila mkopo unaotolewa, kuna simulizi ya uwajibikaji inayohitaji kuendelezwa.

Katika robo ya tatu ya mwaka inayoishia Machi 31, 2026, mengi yamefanyika na kuacha alama chanya katika safari ya HESLB. Tukio lililojitokeza kwa uzito zaidi ni HESLB kupokea tuzo tatu ndani ya kipindi cha roboo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/2026. Tuzo hizi ni kiashiria cha kutambua juhudi za HESLB katika kuimarisha ushirikiano na wadau wa kimkakati pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma.

Miongoni mwa tuzo hizo, ya kwanza ilitolewa katika kilele cha Mkutano wa Mwaka na Maonesho ya Anuani za Makazi (TACPA) tarehe 08 Februari, 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es salaam, Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angela Kairuki ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba. Tuzo hiyo ilitolewa kwa HESLB kwa kutambua ubunifu na uwazi katika usimamizi wa mifumo yake.

Mnamo tarehe 10 Februari, 2026, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHESLB) iliipatia tuzo HESLB iliyokabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mhe. Rashid Hadid Rashid, akimwakilisha Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Lela Mohammed Mussa. Tuzo hiyo iliyopokelewa na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, inaonesha kuthamini mchango wa HESLB katika kuendeleza sekta ya elimu ya juu hapa nchini kupitia ushirikiano wenye tija.

Tuzo ya tatu ni kutoka Serikali Mtandao (eGA) iliyotolewa mnamo tarehe 19 Februari, 2026, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) jijini Arusha na kukabidhiwa kwa HESLB na mgeni rasmi, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dkt. Moses Kusiluka. Tuzo hiyo ilitolewa kuashiria kutambua hatua kubwa zilizopigwa na HESLB katika matumizi ya mifumo ya kidijitali ili kurahisisha huduma kwa wanufaika.

Mafanikio haya si tu ishara ya juhudi za ndani ya taasisi, bali pia ni kielelezo cha dhamira ya HESLB katika kuhakikisha inatoa huduma bora, zenye ufanisi na zinazoendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia. Kupitia uwekezaji katika mifumo ya kidijitali, taasisi imeendelea kuwafikia wanafunzi wengi zaidi kwa urahisi, uwazi na kwa wakati.

Zaidi, ya yote, tuzo hizo zinaimarisha imani ya wadau kwa HESLB na kuthibitisha kuwa ushirikiano wa karibu baina ya taasisi na washirika wake ni nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya elimu ya juu nchini Tanzania.

HESLB inaendelea kusonga mbele kwa kasi, ikiahidi kuendeleza ubunifu, uwajibikaji na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi mwenye sifa anapata fursa ya kufikia ndoto zake za elimu ya juu.

Meza ya Mwenyekiti inaungana na Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwakumbusha wanufaika wote kwamba uzalendo hauishii kwenye maneno tu, bali unapaswa kuonekana kwa matendo. Kulipa mkopo wako ni kuchangia elimu ya Mtanzania mwingine, na ni kushiriki moja kwa moja katika kujenga taifa lenye wataalamu, wabunifu na viongozi wa kesho wanaojiamini.

Sambamba na hilo, HESLB imeboresha mifumo yake ili kurahisisha huduma, na hivyo wanufaika wanaweza kupata ankara zao (loan statements) na kufanya malipo ya madeni yao yaliyoiva kwa urahisi na haraka kupitia mfumo wa LIPA.
Endelea kufuatilia HESLB Yako kwa taarifa zaidi, mafanikio na simulizi zinazoakisi mabadiliko chanya katika sekta ya elimu.




Adolf Mkenda
Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

# 10 wapata ufadhili shahada ya uzamili katika sayansi ya takwimu na akili unde

Dodoma, Jumatano, Februari 25,2026

SSerikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza kutoa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Takwimu (Data Science), Akili Unde (Artificial Intelligence) na Sayansi Shirikishi kupitia mpango wa Samia Scholarship Extended (SSE DS/AI+).

Hatua hiyo imeanza kwa wanafunzi kumi (10) waliopata ufadhili wa kusoma katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) iliyopo jijini Arusha. Aidha, wanafunzi wengine 10 wanatarajiwa kusoma masomo kama hayo katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya India (Indian Institute of Technology Zanzibar IIT Madras), kampasi ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, alisema uamuzi wa kusomesha wanafunzi hao katika ngazi ya Shahada ya Uzamili unatokana na mahitaji ya taifa katika eneo la teknolojia na ubunifu.

Waziri Mkenda alisema Serikali imetenga TZS 5 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo.
"Vyuo tunavyopeleka wanafunzi wa Samia Scholarship AI/DS+ vinatoa mafunzo kwa vitendo katika makampuni ya teknolojia, na vinaendelea kudahili wanafunzi wetu," alisema Prof. Mkenda, na kufafanua kuwa wanafunzi waliopata ufadhili wanatoka katika shule za Serikali na zisizo za Serikali.

Waombaji kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili, huchaguliwa kupitia mfumo wa maombi, tofauti na ngazi ya Shahada ya Awali ambapo wanafunzi huchaguliwa kulingana na ufaulu wao wa juu.

Waziri Mkenda alitumia fursa hiyo kuwaalika wadau mbalimbali kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuchangia katika mfuko wa Samia Scholarship, akisisitiza kuwa Serikali imeamua kuongeza nguvu katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), huku akisema juhudi hizo zinaonekana kupitia ujenzi wa shule maalum za wasichana za sayansi katika kila mkoa, upendeleo wa mikopo kwa wanafunzi wa sayansi kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, pamoja na utoaji wa ufadhili kupitia Samia Scholarship kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita.

Prof. Mkenda pia aliwataka wanafunzi waliopata ufadhili ngazi ya Shahada ya Kwanza kuangalia majina yao katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, www.moe.go.tz, tovuti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) http://www.costech.or.tz na na ya Taasisi ya Afrika ya Sayansi ya Teknolojia ya Nelson Mandela http://www.nm.aist.ac.tz

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa NM-AIST, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema mpango wa Samia Scholarship Extended (SSE DS/AI+) ni uwekezaji wa kimkakati unaolenga kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani, huku ukitoa fursa ya wanafunzi kubadilishana uzoefu kimataifa kutokana na hadhi ya taasisi hiyo.



**Dkt. Bill Kiwia**
*Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB*

# HESLB kuja na Kampeni ya 'Kiduchu'

Dar es salaam, Jumanne, Machi 10, 2026

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia amesema taasisi hiyo iko mbioni kuzindua Kampeni iitwayo 'Kiduchu' inayotarajiwa kuwahamasisha wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kurejesha mikopo yao kidogokidogo badala ya kutorejesha kabisa kwa muda mrefu na hivyo kuwakosesha fursa wanafunzi wengine wahitaji wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Dkt. Kiwia aliyasema hayo katika mahojiano maalum kupitia Kituo cha Televisheni cha Channel Ten ambapo alipata fursa ya kuzungumzia safari ya mafanikio ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika hatua za kutathmini HESLB ilipotoka, ilipo na inapoelekea.

Katika kipindi hicho kiitwacho Twende Pamoja kwa Matokeo ya Haraka, Dkt. Kiwia alizungumzia masuala mbalimbali yanayoainisha mafanikio katika utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo hususan ndani ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huku akisema kupitia 'Kiduchu' wanufaika ambao mikopo yao imeiva, wataweza kurejesha kuanzia kiwango cha TZS 5,000/-.

Dkt. Kiwia alibainisha kuwa kupitia kampeni mbalimbali zilizopita ikiwemo Sifurisha na Fichua; HESLB imefanikiwa kukusanya fedha kutoka kwa wadau na zaidi imefanikiwa kuweka hamasa kwa wanufaika wengi hususani waliopo katika Sekta isiyo rasmi kujitokeza na kurejesha mikopo yao. Alifafanua kuwa Kampeni ya Fichua iliyozinduliwa mwezi Juni, 2024, imewezesha kukusanya kiasi cha TZS 6 bilioni hadi kufikia Machi 2026 kutoka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu 925 ambao wamefichuliwa na kuanza kurejesha mikopo yao.

# HESLB na CIT zasaini makubaliano ya mashirikiano




Arusha, Alhamisi, Januari 29, 2026

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) Dkt. Bill Kiwia Kiwia na Mkurugenzi wa Compassion International Tanzania (CIT), Bi. Mary Lema wamesaini tamko la nia ya kushirikiana (Statement of Intention to Collaborate) ili kuweka utaratibu madhubuti wa kuwatambua wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu ili wapewe kipaumbele katika utoaji wa Mikopo.


Dkt. Kiwia alifanya ziara katika Ofisi za Makao Makuu ya Compassion International Tanzania (CIT) zilizopo jijini Arusha, ikiwa ni moja ya mikakati ya HESLB ya kutafuta na kuingia katika ushirikiano rasmi na wadau wa kimkakati ili kuongeza vyanzo mbadala vya ufadhili kwa wanafunzi katika elimu ngazi ya kati na elimu ya juu nchini.

Dhana hii inaendana na maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha vijana wa kitanzania wanafikia ndoto na malengo yao ya kielimu bila vikwazo.

Mashirikiano haya yanatarajiwa kuwezesha kupatikana kwa vyanzo mbadala vya rasilimali fedha kwa ajili ya kuongeza wigo wa wanufaika wa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Yatima na wanaotoka katika Kaya masikini ambao wana sofa na kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Compassion International Tanzania (CIT) imekuwa na utaratibu wa kuratibu upatikanaji wa wahisani kwa ajili ya kuwasomesha watoto wanaotoka katika kaya za kipato cha chini na jamii za pembezoni kuanzia ngazi ya shule za msingi hadi elimu ya juu.

# HESLB yavuka malengo ya makusanyo Januari - Machi



Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imefanikiwa kuvuka malengo yake ya makusanyo kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo katika kipindi cha miezi mitatu Januari hadi Machi, 2026, hali inayoongeza fursa ya waombaji wa mikopo hiyo kuongezeka.

Kwa mujibu wa taarifa ya HESLB, makusanyo yameongezeka kutoka kwa wanufaika wake, jambo linaloleta faraja kwa taasisi hiyo.

"Miezi mitatu ya Januari hadi Machi, Bodi ililenga kukusanya shilingi bilioni 18.3 kwa kila mwezi, lakini mwezi Januari zimekusanywa shilingi bilioni 20.4, mwezi Februari bilioni 19.4 na mwezi Machi bilioni 20.9," imeeleza taarifa hiyo.

Mafanikio ya makusanyo hayo yametokana wa mwamko wa wanufaika wa mikopo ya elimu kuanza kulipa mikopo yao kwa hiari, baada ya kuhitimu na kuwa na vipato kwa kuajiriwa au kujiajiri wenyewe.

Vilevile, waajiri kutoa taarifa za wanufaika pindi wanapoanza kazi katika taasisi wanazozisimamia, jambo linaloiwezesha Bodi kuongeza makusanyo yake.

Sanjari na hilo, kuimarisha kwa mifumo ya kiteknolojia ambapo sasa mifumo inasomana, imesaidia sana kuongeza makusanyo kutoka kwa wanufaika.

Takwimu zinaonyesha wanufaika 539,103 ambao mikopo yao imeiva wamekopeshwa jumla ya shilingi trilioni 2.76, katika fedha hizo, Bodi imefanikiwa kukusanya trilioni 1.84 kutoka kwa wanufaika 403,917 ambao wameanza kurejesha mikopo yao huku wanufaika 135,186 waliokopeshwa bilioni 920 wakiwa bado hawajaanza kurejesha mikopo yao.

Pia, katika mwaka wa fedha 2025/2026, kwa miezi tisa, Bodi imefanikiwa kukusanya bilioni 175.9 sawa na asilimia 106.6 ya lengo la kukusanya bilioni 165 kwa miezi hiyo.

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, lengo la makusanyo ya mwaka ni kufikisha shilingi bilioni 220.3, kutokana na mwenendo uliopo wa makusanyo, Bodi inatarajiwa kuvuka lengo na kukusanya bilioni 225 ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha yaani Juni 30, 2026.

HESLB ni taasisi ya kiserikali chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye wajibu wa kutoa mikopo na kukusanya mikopo hiyo kutoka kwa wanufaika wake pindi wanapohitimu masomo yao na kuwa na vipato katika sekta ya umma au binafsi.

"Miezi mitatu ya Januari hadi Machi, Bodi ililenga kukusanya shilingi bilioni 18.3 kwa kila mwezi, lakini mwezi Januari zimekusanywa shilingi bilioni 20.4, mwezi Februari bilioni 19.4 na mwezi Machi bilioni 20.9," imeeleza taarifa hiyo.



# HESLB yatuzwa taasisi kinara matumizi ya mifumo kidigitali

Dar es salaam, Jumapili, Februari 08, 2026

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Angela Kairuki ameipongeza Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kuwa taasisi kinara na ya kidigitali katika utoaji wa huduma na utendaji wa kila siku na kuikabidhi tuzo ya kutambua mchango wake katika matumizi ya anwani za makazi.

Waziri Kairuki ambaye amemwakilisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, ameyasema hayo alipotembelea banda la HESLB kwenye Maonesho yaliyoenda sambamba na Mkutano wa Kimataifa wa Mwaka wa Anwani za Makazi na Teknolojia ya Huduma za Posta (TACPA) yaliyofanyika Jumapili, Februari 08, 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Aidha, Mhe. Waziri Kairuki ameiagiza HESLB kuongeza kasi ya makusanyo ya mikopo ya wanafunzi ili kuongeza mchango wake katika utoaji wa mikopo ya wanafunzi ambao wanaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

"Ningependa kuona kiasi cha makusanyo kinaongezeka … hii itasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali na kuwezesha wanafunzi wengi zaidi kujiunga na elimu ya juu", amesema Mhe. Kairuki.

Licha ya maonesho, HESLB pia ilishiriki katika kongamano kuhusu Nafasi ya Anwani za Makazi katika ukuaji wa Sekta mbalimbali na kisha kuendelea kwenye majadiliano kuhusu jinsi ambayo HESLB imetumia anwani za makazi na changamoto zilizojitokeza wakati wa maombi ya mikopo kwa mwaka 2025/2026 kuanzia Julai 15, hadi Septemba 15, 2025.

HESLB ni miongoni mwa taasisi zinazotumia anwani ya makazi hususan katika huduma ya maombi ya mikopo kwa wanafunzi kikiwa ni kipengele muhimu kuanzia mwaka wa masomo 2025/2026 ambacho kimewekwa kuwa ni moja ya taarifa ya msingi inayohitajika kutoka kwa mwombaji na wazazi wake kabla ya kumpangia mkopo stahiki.

Washiriki kutoka ndani na nje ya nchi wametumia jukwaa hilo la siku nne kuanzia Februari 5 hadi 8, 2026 ili kujadili kwa pamoja mafanikio, changamoto na kubadilishana uzoefu miongoni mwa wadau kwa lengo la kuboresha eneo la anwani za makazi na teknolojia ya huduma za Posta likiwa na kauli mbiu isemayo, "Anwani Mahiri na Ubunifu wa Huduma za Posta kwa Ukuaji Jumuishi.

Mkutano na Kongamano hilo Imefanyika kwa mara ya pili na kujumuisha washiriki 1, 000 kutoka nchi mwenyeji Tanzania na wageni kutoka Guinea, Burkina Faso, Korea ya Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Rwanda na Malawi.

"Ningependa kuona kiasi cha makusanyo kinaongezeka … hii itasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali na kuwezesha wanafunzi wengi zaidi kujiunga na elimu ya juu", amesema Mhe. Kairuki.



**Jumatano,Januari 7, 2026, Dar es salaam:** Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdullah (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa HESLB, Bw. Amani Kakana (hayupo pichani) alipotembelea banda la HESLB katika Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar (ZITF) yaliyofanyika katika viwanja vya Dimani kuazia Januari 1- 16, 2026.




**Jumatano,Januari 14,2026, Dar es salaam:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt Bill Kiwia (katikati) pamoja na Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo na Ruzuku za wanafunzi nchini Malawi (HESLGB), Dkt. Dennis Khasu (wa pili kushoto), mara baada ya kikao cha majadiliano baina ya taasisi hizo mbili kilichofanyika katika ofisi za HESLB, jijini Dar es salaam.




**Alhamisi, Januari 29,2026, Arusha:** Mkurugenzi wa HESLB Dkt. Bill Kiwia (kushoto) pamoja na Murugenzi wa Compassion International Tanzania Bi. Mary Lema wakionesha hati za makubaliano waliyosaini.




**Alhamisi, Januari 29,2026, Dodoma:** Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi (aliyekaa katikati) akiwa na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Dkt. Maryam Ismail (kushoto kwake) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt Bill Kiwia katika picha ya pamoja na Menejimenti ya HESLB baada ya tukio la uzinduzi wa huduma ya Akili Unde 'BwanaBoom'. Huduma hiyo inapatikana kwenye tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz na akaunti ya kila mwanafunzi mnufaika (SIPA).




**Jumapili, Machi 08, 2026, Dar es salaam:** Baadhi ya watumishi wanawake wa HESLB wakiwa katika maandamano ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Mburahati - Barafu, jijini Dar es salaam. Mgeni Rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Mhe. Albert Chalamila.




**Alhamisi Machi 05,2026, Dar es salaam:** Watumishi wanawake wa HESLB katika picha ya pamoja na wanafunzi wa kike baada ya kutembelea na kugawa taulo za kike kwa wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Temeke. Tukio hili lilikuwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 08, 2026.



**Jumamosi, Machi 14, 2026, Dar es salaam:** Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Lazaro Londo (wa tano kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, Prof. Hamisi Dihenga (wa nne kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia (wa tatu kulia) katika picha ya pamoja na wadau wa kimkakati wa masuala ya elimu na fedha katika futari iliyofanyika katika hoteli ya Hyatt Regency, jijini Dar es salaam.




# HESLGB ya Malawi yafanya ziara ya mafunzo HESLB

Dar es Salaam, Jumatano, Januari 14, 2026

Menejimenti ya Bodi ya Mikopo na Ruzuku za Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini Malawi (Higher Education Students' Loans and Grants Board - HESLGB) imefanya ziara ya mafunzo kwa kutembelea Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania (HESLB) katika ofisi zake zilizopo eneo la TAZARA, jijini Dar es Salaam.

Ziara hiyo ililenga kupeana mafunzo, kubadilishana uzoefu na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili zinazotekeleza majukumu yanayofanana katika kugharimia wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu.

Akielezea madhumuni ya ziara hiyo, Mtendaji Mkuu wa HESLGB, Dkt. Denis Khasu, alisema kuwa lengo kuu la ziara yao lilikuwa ni kuifahamu HESLB kwa kina na kujifunza namna inavyosimamia mikopo ya wanafunzi. Dkt. Khasu alibainisha kuwa, anaamini pande zote mbili zinakumbana na changamoto zinazofanana katika utoaji wa mikopo, urejeshaji na ufuatiliaji wa marejesho, na akaongeza kuwa upo umuhimu kwa taasisi hizo mbili kubadilishana uzoefu na kujadili njia bora za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza ili kusonga mbele kwa ufanisi.

Awali, akitoa neno la ukaribisho, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alieleza majukumu ya HESLB ya kisheria na mchango wake katika kuwezesha ugharimiaji wa elimu ya juu nchini Tanzania huku akifafanua kuwa HESLB ina dhamana ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa vyuo vya elimu ya juu na vya kati, pamoja na kusimamia urejeshaji wa mikopo hiyo kwa ajili ya uendelevu wa mfuko wa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi.

Dkt. Kiwia pia alieleza kuhusu mifumo mbalimbali ya TEHAMA iliyobuniwa na HESLB kwa ajili ya usimamizi wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu. Alisema kuwa mifumo hiyo ya kidijitali imeimarisha ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma, na kwamba imekuwa nyenzo muhimu katika kusimamia mikopo ya wanafunzi.

Kikao kati ya HESLB na HESLGB kiliweka msingi wa mwendelezo wa kubadilishana maarifa, kujifunza kwa pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Malawi ambazo ni miongoni mwa nchi wanachama katika Shirikisho la Taasisi za serikali zinazogharimia wanafunzi barani Afrika (AAHEFA).




# HESLB, CRDB Bank Foundation na Basil Link zakubaliana kuwezesha wanafunzi

**Dar es Salaam, Jumatano, Februari 18, 2026**

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), CRDB Bank Foundation na kampuni ya Basil Link zimeingia katika makubaliano rasmi ya ushirikiano yanayolenga kuwawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu kupata ujuzi wa kidigitali, elimu ya ujasiriamali na elimu ya fedha.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika hafla ya uzinduzi wa programu hiyo katika Ofisi za Makao Makuu ya Benki ya CRDB, jijini Dar es Salaam ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa CRDB, Bw. Frederick Nshekanabo, ambaye alieleza kuwa ushirikiano huo ni hatua muhimu katika kujenga kizazi chenye maarifa na ujuzi unaoendana na mahitaji ya sasa ya dunia ya kidigitali.

"Tunataka kujenga uchumi wa kidigitali ambao ni kichocheo muhimu cha maendeleo kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.", alisema Bw. Nshekanabo.

Aidha, Bw. Nshekanabo aliwataka wanafunzi wa vyuo vikuu kutumia fursa hiyo kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kupata kompyuta ili kurahisisha kujifunza vyuoni na kuongeza kuwa kupitia programu hiyo, wanafunzi watanufaika na elimu ya fedha, mafunzo ya ujasiriamali, ushauri elekezi pamoja na fursa za mikopo nafuu akibainisha kuwa fursa zitakazotolewa kupitia programu hiyo, zitasaidia wahitimu kurejesha mikopo ya elimu ya juu kwa wakati, na hivyo kuwezesha vijana wengine kunufaika.

Bw. Nshekanabo alieleza kuwa kupitia ushirikiano na Bodi ya Mikopo, wataweza kuwafikia kwa urahisi zaidi wanufaika wa mikopo waliopo vyuoni na kuwaandaa kupitia programu hiyo kwa maisha baada ya kuhitimu masomo yao na aliwakumbusha vijana kuwa kuhitimu chuo bila kuwa na mawazo ya ubunifu yatakayowawezesha kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidigitali haitoshi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Upangaji na Utoaji Mikopo wa HESLB, Dkt. Peter Mmari, alisema HESLB ipo tayari kushirikiana na taasisi binafsi katika kujenga uchumi wa kidigitali na kuwawezesha vijana wa vyuo vikuu. Dkt. Mmari alieleza kuwa Serikali imewekeza kwa vijana kupitia elimu ya kati na ya juu kwa zaidi ya miaka 20, ambapo hadi sasa takribani TZS 8.2 trilioni zimetolewa kwa wanafunzi takriban 1,000,000 ili kuwawezesha kufikia ndoto zao.

Dkt. Mmari alisisitiza umuhimu wa mashirikiano na taasisi mbalimbali, zikiwemo za binafsi, kupitia mifumo ya kidigitali ili kuwafikia wanufaika wa mikopo walioajiriwa na taasisi hizo na kurahisisha ukusanyaji wa mikopo huku akibainisha kuwa kwa sasa takribani TZS 220 bilioni hukusanywa kwa mwaka kutoka kwa wanufaika wa mikopo na kwamba HESLB ipo tayari kushirikiana na CRDB Bank Foundation na Basil Link ili kuhakikisha vijana wanapata elimu ya fedha kuwawezesha kutumia vizuri mikopo yao, kuwa wabunifu na kuweza kujiajiri au kuajiri wengine baada ya kuhitimu masomo yao.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa Basil Link, Dkt. Basil Emmanuel, alitoa wito kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kujitokeza kwa wingi kushiriki katika programu mbalimbali zitakazoratibiwa chini ya ushirikiano huo. Alieleza kuwa timu ya taasisi hiyo itaanza kutembelea vyuo vikuu mbalimbali ili kutoa elimu na mafunzo kwa wanafunzi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kushindana katika soko la ajira na kujiajiri katika mazingira ya uchumi wa kidigitali.

Utekelezaji madhubuti wa makubaliano haya kwa pande zote tatu unalenga kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na kupanua wigo wa fursa zinazowafikia kwa wakati na kwa ufanisi. Wanafunzi watanufaika na ujuzi utakaowawezesha kufikia malengo yao ya kitaaluma na kiuchumi, na hivyo kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa.




# Watumishi wa HESLB watembelea wafungwa Gereza Kuu la Isanga

"Tuwakumbuke watu walio katika changamoto, kama vile wafungwa kwani wanahitaji upendo na faraja kutoka kwetu", amesema Bi. Octavia.

Dodoma, Jumatano, Machi 18, 2026

Watumishi wa HESLB Ofisi ya Dodoma, wamefanya matendo ya huruma kwa kupeleka msaada wa vitu mbalimbali katika Gereza Kuu la Isanga lililopo jijini Dodoma.

Meneja wa HESLB Ofisi ya Dodoma, Bi. Octavia Seleman amesema wameamua kutoa msaada katika gereza la Isanga ikiwa ni sehemu ya sadaka na matendo ya huruma katika kipindi cha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani na Kwaresma ili kuwakumbuka watu walio katika changamoto na wanaohitaji faraja.

"Tuwakumbuke watu walio katika changamoto, kama vile wafungwa kwani wanahitaji upendo na faraja kutoka kwetu", alisema Bi. Octavia.

Watumishi hao wa HESLB walipokelewa na mwakilishi wa Kamishna wa Magereza, ACP Atu Juvenile Namwata ambaye aliwashukuru kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa Magereza kwa moyo wao wa kujitoa na sadaka walizozitoa gerezani hapo.

"Kwa sasa Jeshi la Magereza linajitegemea katika kujiendesha, pamoja na miradi mingine … pia tunashukuru sana kwa sadaka zenu maana zinaongezea katika mahitaji ambayo wanafunzi wetu (akimaanisha wafungwa) hapa wanahitaji", alisema ACP Namwata na kuongeza, "Tunawakaribisha sana hata kuja tu kuongea nao ili kuwapa maneno ya faraja maana yanawajenga kisaikolojia".

# Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani 2026: HESLB Yagawa Taulo za Kike Temeke Sekondari






Dar es salaam, Alhamisi, Machi 5, 2026

HESLB imetembelea na kugawa taulo za kike kwa wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Temeke jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yanayoadhimishwa kila mwaka tarehe 08 Machi.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu wa HESLB, Bi. Suzana Kiwelu alisema kuwa lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuwapa moyo wanafunzi wa kike katika safari yao ya masomo pamoja na kuwapatia zawadi itakayowasaidia kusoma kwa furaha na kujiamini huku akibainisha kuwa mabadiliko ya kibaiolojia wanayopitia wanafunzi wa kike ni ya kawaida na hayapaswi kuwa kikwazo katika kufikia ndoto zao za kielimu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Temeke, Mwl. Ingia Mtenga alishukuru HESLB kwa kuwakumbuka wanafunzi wa kike wa shule hiyo na kutoa zawadi hizo. Amesema taulo hizo zitakuwa chachu ya kuwahamasisha mabinti kusoma kwa bidii bila kukatishwa tamaa na changamoto zozote zinazoweza kuwazuia kuhudhuria masomo.

Katika tukio hilo, jumla ya maboksi 105 ya taulo za kike yenye thamani ya shilingi milioni 6 yalikabidhiwa kwa wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Temeke, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya jinsia ya HESLB pamoja na kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Sambamba na tukio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alishiriki katika hafla ya futari iliyoandaliwa na watumishi wanawake wa HESLB katika Hoteli ya King Jada iliyopo jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya shamrashamra kuelekea maadhimisho ya siku ya wanawake duaniani.

Akizungumza katika hafla hiyo ya futari, Dkt. Kiwia aliwapongeza wanawake wafanyakazi wa HESLB kwa kuandaa tukio hilo muhimu litakaloacha alama katika sikukuu ya wanawake kwa mwaka 2026 akieleza kuwa, ni fursa nzuri ya kukutana na kubadilishana mawazo na kuendelea kuimarisha umoja ndani ya taasisi.

Dkt. Kiwia pia alisisitiza kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika kuifikia Dira ya Taifa 2050, akieleza kuwa maendeleo endelevu hayawezi kupatikana bila ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Aidha, Dkt. Kiwia alibainisha kuwa kila mwanamke ana haki ya kupata fursa sawa katika elimu na ajira, na kwamba mafanikio ya jamii kwa ujumla yanategemea ushirikiano wa watu wote, wakiwemo wanawake.




# HESLB na Taasisi zinazofadhili Wanafunzi zalenga kuimarisha Ushirikiano

Arusha, Alhamisi, Machi 26, 2026

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imekabidhi vyeti vya usajili na utambuzi kwa taasisi 305 zinazofadhili masuala ya elimu kwa watoto na vijana ili kuonesha umuhimu mkubwa wa ushirikiano kati ya HESLB na wadau wa ufadhili wa elimu, ambapo kwa pamoja wanaweza kuwafikia wanafunzi wengi zaidi wenye uhitaji na kuwawezesha kupata elimu ya juu, hatua inayochochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

Utoaji wa vyeti hivyo vya usajili kwa wafadhili wa elimu unafuatia maboresho ya namna ya kuwatambua wafadhili halisi kwa kuwasilisha taarifa zao kwenye mfumo wa maombi ya mikopo wa HESLB, utaratibu ulioanza mwaka huu wa masomo 2025/2026 ukilenga kuimarisha ushirikiano na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na ugharimiaji wa wanafunzi.

Akifungua kikao kazi baina ya pande hizo mbili ambacho kilifanyika katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, jijini Arusha (NM-AIST), Mgeni rasmi ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alibainisha kuwa kikao hizo kilikuwa kimeandaliwa mahsusi ili kujenga ushirikiano madhubuti kati ya HESLB na taasisi zinazofadhili wanafunzi kwa lengo la kuboresha ufanisi wa utendaji na kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wanapata fursa ya elimu ya juu.

Dkt. Kiwia alizipongeza taasisi hizo kwa kuona umuhimu wa kuwasomesha mamia ya watoto na vijana wanaotoka katika kaya zenye kipato cha chini au zenye changamoto mbalimbali za kiuchumi na kijamii, huku akisisitiza kuwa mchango wa taasisi za ufadhili wa elimu ni muhimu kwa maendeleo ya taifa na ameongeza kuwa kikao hicho kitakuwa ni endelevu na kitafanyika kila mwaka ili kuimarisha mahusiano, kuboresha huduma kwa wanafunzi, na kuangalia namna bora ya kushirikiana na taasisi zinazofadhili wanafunzi kuanzia ngazi ya shule za msingi na sekondari.

"Tunaamini kuwa kwa kuimarisha ushirikiano huu, tutafanikiwa kuwafikia wanafunzi wengi zaidi wenye uhitaji, kuunganisha nguvu zetu katika kuwahudumia, na kuweka misingi imara ya maendeleo ya elimu ya juu nchini," alisema Dkt. Kiwia.

Aidha, Dkt. Kiwia aliishukuru Serikali kwa jitihada kubwa za kuwekeza katika elimu ya juu ambapo zaidi ya TZS 3.6 trilioni zimetolewa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Alieleza kuwa tangu kuanzishwa kwa HESLB, zaidi ya Watanzania milioni moja (1) wamenufaika na mikopo ya elimu ya juu, jambo linaloonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuwawezesha vijana kufikia ndoto zao za kielimu.

Akizungumzia matarajio ya HESLB baada ya kikao hicho, Dkt. Kiwia alisema matokeo ya kikao kazi hicho yatawezesha kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa sahihi na kuweka kumbukumbu kidijitali kwa ufanisi mkubwa kwa kushirikiana na wadau ili kuwafikia wanafunzi wengi Zaidi. Aliongeza kuwa hatua hiyo itawezesha kupanua wigo wa ufadhili wa elimu ya juu, pamoja na kupokea maoni yatakayosaidia kuboresha mifumo ya ufadhili na utoaji wa huduma kwa wanafunzi.

Awali, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Suzana Augustino kwa niaba ya Makamu Mkuu wa NM-AIST, aliishukuru HESLB kwa mchango wake katika elimu akiweka bayana kuwa yeye pia ni miongoni mwa wanufaika wa mikopo hiyo. Alisema wanafurahi kwa Taasisi hiyo kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa kikao kazi hicho muhimu na aliwakaribisha washiriki wote na wadau mbalimbali kufika katika taasisi hiyo kwa ajili ya kujifunza na kubadilishana uzoefu. Prof. Suzana alibainisha kuwa lengo la taasisi hiyo ni kuwa kituo kikubwa cha utafiti wa kisayansi na ubunifu.




# HESLB Yafuturisha Wadau wa Kimkakati Zanzibar na Dar es Salaam

Machi 11 & 14, 2026

Katika kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na wadau wake wa kimkakati, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetumia Mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan kuandaa hafla za futari Zanzibar na Dar es Salaam kwa lengo la kuwaleta pamoja wadau muhimu na kujadili maendeleo ya utoaji wa huduma kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Hafla ya Futari Zanzibar ilifanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahr, ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. Suleiman Masoud Makame, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Tukio hilo liliwakutanisha viongozi mbalimbali wa serikali, taasisi za elimu pamoja na wadau wa maendeleo waliopata fursa ya kubadilishana mawazo na uzoefu kuhusu namna bora ya kuendelea kuboresha sekta ya elimu ya juu.

Mhe. Makame aliwataja Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa viongozi wanaoongoza nchi kwa umakini mkubwa.

“Tunamshukuru Mwenyezi Mungu na kumwomba aweze kuwapa viongozi wetu moyo wa upendo na imani”, alisema Mhe. Makame.

Kwa upande wa Dar es Salaam, hafla ya futari ilifanyika katika hoteli ya Hyatt Regency Dar es Salaam, (The Kilimanjaro), ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Lazaro Londo. Katika hotuba yake, Mhe. Londo alisisitiza umuhimu wa kuendelea kushirikiana kwa karibu kati ya taasisi za umma na wadau binafsi ili kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata fursa sawa za elimu.

Awali, akitoa maneno ya utangulizi na shukrani kwa wadau wote walioshiriki katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia alisema kuwa HESLB imekuwa na utaratibu wa kuandaa futari maeneo mbalimbali ya nchi na kushirikiana na wadau wake kwa lengo la kuimarisha mshikamano na ushirikiano.

“Tumekuwa na utaratibu kama huu miaka ya hivi karibu kwa lengo la kufahamiana, kuifahamu taasisi yetu na kuimarisha mshikamano”, alisema Dkt. Kiwia.

Hafla za futari zimeendelea kuwa jukwaa muhimu la kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya HESLB na wadau wake, pamoja na kutoa fursa ya kutathmini mafanikio yaliyopatikana na kuweka mikakati ya pamoja kwa ajili ya maendeleo endelevu ya elimu ya juu nchini Tanzania.

“Tunamshukuru Mwenyezi Mungu na kumwomba aweze kuwapa viongozi wetu moyo wa upendo na Imani”, amesema Mhe. Makame.

# WASILIANA NASI:

## DODOMA
Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## ARUSHA
NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712,Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

## MWANZA
PSSSF Plaza, ghorofa ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

## ZANZIBAR
Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA
PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## MBEYA
Jengo la CAG, Ghorofa ya Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA
NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya tatu,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo,Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,
15471-Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz